# Dkt. Ntuli A. Kapologwe

Mkurugenzi wa huduma za Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe

# OFISI YA RAIS -TAMISEMI

# MAJUKUMU YA IDARA YA AFYA, USTAWI WA JAMII NA LISHE

# NA

# KAMATI ZA USIMAMIZI WA SHUGHULI ZA AFYA, USTAWI WA JAMII NA LISHE MKOA

# Dira na Dhamira ya Idara ya Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe

## DIRA NA DHAMIRA

### 1.1.1 DIRA

Dira ya Idara ya Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe OR – TAMISEMI ni kuwa Idara ya mfano katika kuratibu utoaji wa huduma za Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe, zenye ubora wa hali ya juu kwenye sekretariati za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

### 1.1.2 DHAMIRA

Dhamira ya Idara ya Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe OR – TAMISEMI ni kuziwezesha Sekretarieti za Mikoa pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa ili ziweze kutoa huduma bora za Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe kwa kupitia Uratibu, uandaaji wa mipango, usimamizi saidizi, ufuatiliaji na tathmini.

# Utekelezaji wa Majukumu ya Idara ya Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe

- Ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015.
- Sera ya Afya ya mwaka 2007,
- Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi (MMAM) 2007 – 2017
- Mpango Mkakati wa Nne wa Sekta ya Afya (Health Sector Strategic Plan IV 2015 – 2020)
- Mpango Mkakati wa Kuboresha Huduma za Uzazi na Afya ya Mama na Mtoto (ONE PLAN II – 2016 – 2020)
- Mpango Mkakati wa Nne wa UKIMWI wa Sekta ya Afya (Health Sector HIV Strategic Plan IV – 2017 – 2022) n.k
- Malengo endelevu ya Maendeleo (SDG) 2015 -2030
- Maagizo mbalimbali ya Serikali

# Malengo ya uanzishwaji wa Idara ya Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe (Februari, 2015)

**Lengo Kuu;**

Kuzisimamia Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ili ziweze kutoa huduma bora za afya, Ustawi wa jamii na Lishe kwa kufanya uratibu, uandaaji wa mipango na Bajeti, usimamizi saidizi, ufuatiliaji na tathmini. Sambamba na hilo inahusika na usambazaji wa sera, miongozo ya utekelezaji pamoja na kufanya tafiti na kusambaza matokeo yake.

# Malengo Mahsusi ya uanzishwaji wa Idara ya Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe…………

- Kusimamia Misingi ya utawala bora katika ufuatiliaji na tathmini ya utoaji wa huduma za afya katika sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa

- Kutafsiri Sera za Kitaifa na Kimataifa na miongozo mbalimbali inayohusiana na maendeleo ya sekta ya Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe

- Kushiriki katika uandaaji wa Sera na Miongozo mbalimbali

- Kutafsiri na kubadilisha nadhalia (theories) kuwa vitendo.





**Figure 1:** Proposed Conceptual Theory of Change (ToC) framework for the DHFF program implementation in Tanzania





**Figure 1:** Nadharia ya Ukarabati ya Vituo vya kutolea huduma za afya na matokeo tarajiwa


# **Majukumu ya Msingi**….

- Kufanya tafiti na machapisho juu ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali (kutekeleza, Kuandika na Kushapisha).
- Kuratibu Miradi/Programu za Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe katika Mikoa na MSM
- Kuratibu na Kuhuisha Takwimu za Afya Ustawi wa Jamii na lishe
- kuratibu ushiriki wa jamii katika utekelezaji wa Miradi ya Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe
- Kutoa mapendekezo juu ya maeneo ambayo yanatakiwa kutengenezewa au kuhuishwa Sera, Sheria  na Miongozo (mf. 3.3.2017, HS guidelines)
- Kuratibu wadau wote wa Afya wanaofanya kazi katika ngazi ya Sekretarieti ya Mikoa na MSM.


# Majukumu ya Msingi: Uratibu wa Wadau




# Majukumu ya msingi: Kutengeneza trends za maoteo



# Maeneo Muhimu yanayo zingatiwa na Idara ya Afya



# Muundo wa Idara ya Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe – OR TAMISEMI



# MAJUKUMU YA RHMT

1. Kushauri Sekretarieti za Mikoa juu ya masuala yahusuyo Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe ili kusaidia kuboresha utoaji wa huduma hizo katika ngazi ya Jamii.
2. Kuhakikisha sera zinatafsiriwa, kutekelezwa kulingana na mipango na bajeti zilizoandaliwa
3. Kuhakikisha kuna mahusiano mazuri baina ya idara ya afya na idara nyingine katika ngazi ya Mikoa na Halmashauri
4. Kuhakikisha uhusiano baina ya Serikali, mashirka binafsi na asasi za kiraia unakuwa imara kwa ajili kuboresha huduma za Afya
5. Kuandaa mipango na taarifa za RHMT
   - Mipango ya kila mwaka
   - Mipango mkakati

# MAJUKUMU YA RHMT……..

6. Kutawanya sera, Miongozo kanuni na nyaraka kwa ajili ya Halmashauri

7. Kuratibu huduma za Lishe na Ustawi wa Jamii katika Mikoa na Halmashauri

8. Kuratibu masuala ya rasilimali watu

- Kuwapangia kutokana na uhitaji
- Kusimamia MSM katika utekelezaji wa majukumu yao

9. Kuhakikisha kuna utoaji wa huduma bora za afya

10. Kufanya ziara za usimamizi shirikishi kwa Hospitali ya rufaa ya Mkoa na Vituo vyote vya kutolea huduma katika Halmashauri

# MAJUKUMU YA RHMT……..

11. Kukabiliana na kupambana na milipuko na majanga

12. Kuhakikisha kwamba kunakuwepo na mifumo ya makusanyo ya mapato katika vituo vya kutolea huduma za afya

13. Kufanya utafiti na kisha kufanya machapisho

14. Kutoa mapendekezo juu ya maeneo ambayo yanatakiwa kutengenezewa au kuhuishwa Sera, Sheria na Miongozo

15. Kuhakikisha kunakuwepo mifumo ya ufuatiliaji kwa magonjwa mbalimbali (Survaillance system)

# MAJUKUMU YA RHMT

16.Msimamizi wa Rasilimali zote zihusuzo Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe ndani ya Mkoa

17. Kuwa Washauri wataalam wa Masuala yote yahusuyo mifumo ya Afya na utoaji wa huduma (Consultant/ Think tank)

18. Kuangalia na kusimamia mtawanyo wa rasilimali wenye tija

19.Nk (kujiongeza)

# Mabadiriko ya kiumiliki na kiutawala kwa Hospitali za Rufaa za Mikoa

- November, 2017. Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alitoa maelekezo juu ya umiliki wa Hospitali za Mikoa

# Mabadiriko ya Kiutawala katika Hospitali za Rufaa za Mikoa

***Tujikumbe kidogo:Karimjee Hall, Tarehe 3-4/11/2016 JAHSRM***





# Tujikumbushe kidogo: Maazimio Kikao cha RMOs & DMOs 2016

| SN | Hoja | Mapendekezo | Muhusika | Muda wa Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|
| 8 | Mfumo wa Uongozi na Utawala wa Hospitali za Rufaa za Mikoa na Kanda na haukidhi haja | 1. Bodi za Ushauri za Hospitali za Mikoa zifanywe kuwa Bodi kamili zenye mamlaka ya kutoa maamuzi na kusimamia utekelezaji<br>2. Waganga wafawidhi wa Hospitali za Rufaa Kanda, Mikoa na Halmashauri watambuliwe kwa vyeo vya madaraka na walipwe mishahara na stahiki husika za madaraka kulingana na kazi ngumu wanazofanya. | WAMJW & OR TAMISEMI | Juni, 2017 |
| 10 | Hospitali za Rufaa za Mikoa hazina uwezo wa kutoa huduma za tiba za kibingwa kama inavyokusudiwa | 1. Serikali itoe vifaa vya uchunguzi kwa angalau hospitali tano za Mikoa ya kimkakati kwa kuanzia<br>2. Kuhamasisha Mpango wa usimikaji vifaa vya uchunguzi katika vituo kupitia ushirikishaji wa sekta Binafsi/ ubia (PPP) uimarishwe katika ngazi zote<br>3. Wizara iandae mpango na bajeti ya mafunzo kwa wataalamu wa usingizi, mionzi na Wataalamu wengine muhimu kwa ajili ya utoaji wa huduma | WAMJW & OR TAMISEMI | Septemba, 2018 |

# Mapendekezo ya Maboresho Mapya

- RHMT itakuwa na Wajumbe 15 ambao watafanya kazi chini ya Katibu Tawala wa Mkoa.

- Kati ya hao wajumbe 6 watafanya kazi chini ya Mganga mfawidhi mpaka watakapokuwa wakihitajika na AAS-Afya/RMO


- Wajumbe wengine wanaweza kupewa uratibu wa shughuli zaidi ya moja kutokana na uhitaji wa kazi husika


- Mganga Mkuu wa Mkoa atakuwa mmoja wa wajumbe wa Bodi ya RRH

- KM Afya atakuwa akiwasiliana moja kwa moja na RAS-Mganga Mkuu wa Serikali katika masuala ya Majanga, milipuko na yale ya dharura , kwa masuala mengine yote atawasiliana kupitia OR-TAMISEMI


- Bodi itatakiwa kuwasilisha masuala yake kwa Waziri wa Afya

# Tujikumbushe: Mfumo wa Afya Tanzania




PO-RALG
MOHCDGEC
Emergence/Outbreak
REGIONAL ADMINISTRATIVE SECRETARY
RHMT (AAS-HEALTH/RMO)
REGIONAL HOSPITAL ADVISORY BOARD (RRHAB)
RNO
RHS
RHO
RSWO
RNuO
RPHARM
RLT
RDO
REGIONAL REFERAL HOSPITAL (RRH)- (MO I/C)
HMIS/ (M&E) FP
RACC
RMFP
RRCHCo
RTLC
RIVO
OTHER COOPTED MEMBERS under RRH


# Namna ya kufanikisha utendaji wa majukumu baada ya mgawanyo mpya




- **Suala la kiuongozi,**
- Ushirikiano
- Busara
- ‘System thinking’
- Uzalendo
- Kufanya mapitio ya Sera na Miongozo ili kuendana na Mabadiriko haya.

# Fursa: KM-WAMJW na NKM (A)- ORTAMISEMI




Who wants change?
Who wants to change?

**Asanteni kwa Kunisikiliza**